- Kuandaliwa kwa Rasimu za Awali za Miswada miwili inayohusu Biashara kupitia Mtandao na Mfumo wa Malipo kupitia Mtandao.
- Tume ya Kurekebisha Sheria ilitoa Elimu ya Sheria kuhusiana na TEKNOHAMA kwa Wadau wa Sekta mbalimbali.

HITIMISHO

TEKNOHAMA imeleta faida kubwa kwa watumiaji na ukuaji wa Uchumi. Pia TEKNOHAMA imeleta changamoto ya umuhimu wa kutungwa kwa Sheria kwani eneo hili kwa muda mrefu limekuwa halina sheria inayosimamia wakati uhalifu ukiendelea kufanyika kwenye sekta mbalimbali.

Ripoti ya Tume imeainisha changamoto zote na kupendekeza maeneo muhimu yanayohitaji kufanyiwa mabadiliko au kutungiwa sheria ambapo baadhi ya sheria zimefanyiwa mabadiliko madogo. Lakini mabadiliko hayo hayakidhi usimamiaji wa matumizi mabaya ya TEKNOHAMA. Ni matumaini ya Tume kuwa Serikali itaendelea kuzifanyia mapitio ya mara kwa mara sheria zinazosimamia TEKNOHAMA ili kwenda sanjari na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

Mawasiliano:

Katibu Mtendaji,

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,

Mtaa wa Luthuli, Kiwanja Na. 8,

S.L.P. 3580,

DAR ES SALAAM – TANZANIA.

Simu: +255 22 2123533

Faksi: +255 22 2123534

Barua Pepe: lrct@lrct.or.tz

Tovuti: www.lrct.or.tz

© LRCT 2010

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

ELIMU YA SHERIA KWA UMMA

MATUMIZI YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO TANZANIA

UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ni Idara inayojitegemea iliyoanzishwa na Sheria ya Bunge Na. 11 ya 1980, Sura 171 [Toleo la 2002]. Sheria hii inaipa Tume mamlaka ya kufanya mapitio ya sheria na kisha kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo ambayo huwasilishwa kwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria na Waziri huwasilisha mapendekezo hayo Bungeni kwa ajili ya utunzi wa sheria. Lengo ni kuzifanya sheria za nchi ziende sanjari na mazingira ya sasa ili kudumisha utawala wa sheria na usimamizi wa haki nchini. Aidha, Tume inaweza kufanya utafiti na kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya iwapo kuna haja ya kufanya hivyo.

Maendeleo ya teknolojia hasa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) duniani ikiwemo Tanzania yamekuwa yakileta changamoto nyingi za Kisheria. Kwa muda mrefu eneo la TEKNOHAMA limekuwa halina sheria maalumu ya kusimamia sekta hii, licha ya kuwa Watanzania wengi hutumia teknolojia hii kwa mawasiliano, elimu na biashara.

Mwaka 2005, Tume ya Kurekebisha Sheria ilianza kufanya utafiti katika eneo hili kwa lengo la kutoa mapendekezo Serikalini ili kuwa na mfumo wa sheria utakaosimamia eneo hili.

CHANGAMOTO ZA KISHERIA ZINAZOLETWA NA TEKNOHAMA

TEKNOHAMA inarahisisha mambo mengi ambayo yanaweza kusaidia kukua kwa uchumi pamoja na kupunguza umaskini kwa wananchi. Watu wengi wamekuwa wakitumia kompyuta, simu na vifaa vingine vya teknolojia ya kompyuta kurahisisha mawasiliano na biashara kupitia mtandao bila kuwepo mfumo wa kisheria.

Matumizi ya TEKNOHAMA yamekuwa yakileta changamoto nyingi zinazohitaji mabadiliko ya kisheria.

Changamoto kubwa ni usalama wa watumiaji wa TEKNOHAMA kwani imerahisisha wahalifu kufanya makosa yao kirahisi zaidi bila ya kuwatambua.

TEKNOHAMA ina upungufu ambapo sheria zilizopo hazijajumuisha vifungu vyenye makosa haya.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

Vile vile Wanawake na watoto wamekuwa ni wahanga wakubwa wa matumizi mabaya ya TEKNOHAMA ambapo haki zao zimekuwa zikikiukwa kupitia tovuti na blogu mbalimbali ulimwenguni kote.

MAENEO YA SHERIA YALIYOATHIRIWA ZAIDI NA TEKNOHAMA

- Sheria zinazosimamia Makosa ya Jinai;
- Sheria zinazosimamia Ushahidi;
- Sheria zinazosimamia Biashara na Fedha.
- Sheria zinazosimamia Mawasiliano;
- Sheria zinazosimamia Watoto;
- Sheria za Madai;
- Sheria zinazosimamia Haki ya Mali iliyotokana na Ubunifu;
- Sheria zinazosimamia Kodi;
- Sheria zinazosimamia Ushindani wa Haki katika Biashara;
- Sheria zinazosimamia Utunzaji wa Taarifa za Siri;
- Sheria zinazosimamia kumbukumbu za Nyaraka.

MAPITIO NA UTAFITI WA SHERIA MBALIMBALI

Mwaka 2005, Tume ilifanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazoathiriwa na matumizi ya TEKNOHAMA ili kubaini maeneo yanayohitaji marekebisho au kutungiwa sheria mpya. Katika kufanya hivyo,Tume iliwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wa sekta ya TEKNOHAMA katika kukusanya maoni na takwimu mbalimbali ili kuandaa Ripoti yenye mapendekezo itakayowasilishwa Serikalini kwa utekelezaji zaidi.

Mwaka 2006, Tume ilikabidhi Ripoti ya Biashara kupitia Mtandao kwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

MAPENDEKEZO YA TUME

Katika Ripoti hiyo Tume ilipendekeza yafuatayo:-

- Kuanzishwa kwa Mfumo wa Sheria utakaosimamia Sekta ya TEKNOHAMA.
- Kutungwa kwa Sheria mpya zitakazosimamia Makosa kupitia Mtandao (Cyber Crimes), Utunzaji wa Taarifa za Siri (data protection), Biashara kupitia Mtandao (E-Commerce) Uthibitisho na Utambulisho kupitia Mtandao (Electronic Signatures).
- Kufanyia marekebisho Sheria ya Ushahidi ili kutambua ushahidi unaotokana na matumizi ya TEKNOHAMA.
- Kuzifanyia marekebisho Sheria zinazosimamia Haki ya Mali iliyotokana na Ubunifu.
- Kuzifanyia marekebisho Sheria zinazosimamia Ushindani wa Haki katika Biashara.
- Kuzifanyia marekebisho Sheria zinazosimamia Kodi.
- Kusaini na Kuridhia Mikataba ya Kimataifa ya Mawasiliano na Mkataba kupitia Mtandao wa Kimataifa wa mwaka 2005.
- Kutoa Elimu ya TEKNOHAMA pamoja na Sheria zake.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI

Baada ya Serikali kuipokea Ripoti hiyo mambo yafuatayo yalifanyika:

- Marekebisho Sheria ya Ushahidi ili kutambua ushahidi wa matumizi ya TEKNOHAMA, kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 2007.
- Marekebisho ya baadhi ya Sheria za Kodi kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2009.
- Idara ya Polisi imeunda Kitengo cha kushughulikia Makosa yatokanayo na matumizi ya TEKNOHAMA.